JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# MWONGOZO WA KAMPENI YA CHANJO ZA MIFUGO ZA RUZUKU KITAIFA KWA MWAKA 2024/2025



**S.L.P 2870**
**40487 DODOMA**
Barua pepe: ps@mifugo.go.tz

**Februari, 2025**



**Dibaji**

Utoaji wa chanjo ni njia rahisi ya kutegemewa na yenye gharama nafuu katika kudhibiti magonjwa ya wanyama. Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kukabili changamoto za magonjwa ya mifugo yanayoathiri afya za wanyama, binadamu na biashara itaimarisha matumizi ya chanjo kwa kufanya Kampeni ya Chanjo ya Mifugo kitaifa. Kampeni hii itafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya Mwaka 2006, Sheria ya Magonjwa ya Wanyama ya Mwaka 2003, Sheria ya Ustawi wa Wanyama na Kanuni mbalimbali zinazosimamia maendeleo ya Sekta ya Mifugo.

Ili kutekeleza Kampeni hii kwa usawa nchi nzima, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeandaa Mwongozo wa Kampeni ya Chanjo za Mifugo za Ruzuku Kitaifa kwa Mwaka wa fedha 2024/2025. Mwangozo huu unaweka utaratibu na kufafanua masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa Kampeni hiyo itakayotekelezwa katika kipindi hicho. Aidha, Mwongozo huu unaainisha mahitaji, majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali watakaoshiriki.

Wadau walioainishwa kwenye mwongozo huu ni pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Vyama vya wafugaji, Watoa huduma wa Sekta Binafsi, Serikali za vijiji pamoja na Wafugaji. Aidha, Mwongozo huu unaainisha usimamizi na upimaji wa ufanisi wa zoezi la chanjo na namna ya kuhakikisha kuwa chanjo inatolewa kwa usahihi.

Mhe. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb)
**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**

**YALIYOMO**

**Dibaji**

**1.0 UTANGULIZI ........................................................ 3**

**2.0 MALENGO YA MWONGOZO HUU ........................................................ 4**

2.1 Lengo kuu la mwongozo ........................................................ 4
2.2 Malengo Mahsusi ya Mwongozo........................................................ 4

**3.0 CHIMBUKO LA MWONGOZO ........................................................ 4**

**4.0 UMUHIMU WA CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO ........................................................ 5**

4.1 Umuhimu wa chanjo........................................................ 5
4.2 Faida za Utambuzi wa mifugo........................................................ 6

**5.0 URATIBU WA KAMPENI YA CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO .............. 6**

5.1 Upatikanaji wa chanjo na vifaa vya kuchanjia........................................................ 6
5.2 Upatikanaji wa Hereni na vifaa vya utambuzi wa Mifugo ........................................................ 7
5.3 Timu za Uchanjaji........................................................ 7
5.4 Bei Elekezi ya chanjo na Uvalishaji Hereni........................................................ 8
5.5 Utaratibu wa kukusanya fedha za Uchanjaji ........................................................ 9
5.6 Gharama za uendeshaji na malipo kwa washiriki wa Kampeni ........................................................ 9
5.7 Usimamizi ........................................................ 9

**6.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA KAMPENI YA CHANJO YA MIFUGO KITAIFA ........................................................ 10**

**7.0 MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI ........................................................ 10**

7.1 Wizara ya Mifugo na Uvuvi........................................................ 10
7.2 Majukumu ya OR-TAMISEMI ........................................................ 10
7.3 Majukumu ya Vituo vya kanda (ZVCs/TVLAs) ........................................................ 11
7.4 Majukumu ya Ofisi za Mikoa (RS) ........................................................ 11
7.5 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ........................................................ 11
7.6 Majukumu ya Msambazaji wa chanjo........................................................ 12
7.8 Majukumu ya Serikali ya Kijiji au Mtaa ........................................................ 12
7.9 Majukumu ya Vyama vya Wafugaji ........................................................ 12
7.10 Majukumu ya mfugaji ........................................................ 13

**8.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO ........................................................ 13**

## 1.0 UTANGULIZI

Tanzania ni moja ya nchi barani Afrika zenye mifugo mingi na hivyo kufanya sekta ya mifugo kuwa na umuhimu mkubwa katika uchumi wa kaya na kuwa na uwezo wa kuchangia sana katika pato la Taifa. Kwa sasa, sekta hii huchangia kiasi cha asilimia 6.7. Mchango huu unaweza kuongezeka iwapo mipango madhubuti itachukuliwa kama inavyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya mwaka 2006 na programmu ya Maendeleo ya Mifugo. Mpaka sasa, Tanzania ina jumla ya ng'ombe milioni 37.9; mbuzi milioni 27.6; kondoo milioni 9.4; nguruwe milioni 3.9; punda wapatao 657,389 na kuku milioni 103.1.

Kama ilivyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya mwaka 2006, moja ya changamoto inayokabili sekta hii ni uwepo wa athari za magonjwa. Magonjwa ya mifugo sio tu yanapunguza uzalishaji bali pia yanaathiri biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi na kudumaza kwa kiasi kikubwa, mchango wa sekta ya mifugo katika kuchangia pato la kaya kwa wafugaji na taifa kwa ujumla. Aidha, baadhi ya magonjwa ya wanyama huambukiza binadamu (*zoonoses*). Hivyo, uwepo wa maambukizi ya magonjwa kati ya mifugo, wanyamapori na binadamu ni suala ambalo linalazimisha uwepo wa mikakati endelevu na shirikishi ya udhibiti wa magonjwa husika.

Udhibiti wa magonjwa ya wanyama hufanyika kwa njia mbalimbali ikiwemo utoaji wa matibabu, utoaji wa chanjo kwa magonjwa ya kipaumbele; kuogesha wanyama kwa kutumia dawa za kuua kupe na wadudu wengine; kuweka karantini na mamlaka husika kwa magonjwa muhimu ya kipaumbele wakati milipuko inapotokea na kuwekwa kwa mikakati ya kuzuia mwingiliano wa kundi moja la mifugo na kundi jingine. Kwa ujumla, utoaji wa chanjo ni njia rahisi, ya kutegemewa na yenye gharama nafuu katika kuzuia magonjwa. Kwa mwaka wafedha 2024/2025 Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepanga kutekeleza kampeni ya chanjo ya Mifugo kitaifa dhidi ya magonjwa matatu ambayo ni Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) kwa nchi nzima, Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) katika mikoa 14 yenye maambukizi ya ugonjwa huu, pamoja na mdondo/kideri kwa kuku kwa nchi nzima. Mikoa itakayo husika na uchanjaji dhidi ya ugonjwa wa

sotoka ya mbuzi na kondoo ni Dodoma, Simiyu, Morogoro, Pwani, Arusha, Mara. Manyara, Lindi, Mtwara, Kilimanjaro,Tanga, singida, Mwanza na Shinyanga.

Aidha, Serikali kwa kutambua umuhimu wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo, imepanga Kampeni hii ya Chanjo Kitaifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 itekelezwe sambamba na utambuzi na uwekaji hereni kwa ng’ombe katika baadhi ya maeneo ambayo ni Mikoa ya Mara, Pwani, Morogoro, Njombe, na Iringa.

## 2.0 MALENGO YA MWONGOZO HUU

### 2.1 Lengo kuu la mwongozo

Mwongozo huu unalenga kuainisha mahitaji, majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali katika zoezi la utoaji wa chanjo yenye ruzuku ya Serikali kitaifa dhidi ya magonjwa ya Homa ya Mapafu ya Ng’ombe (CBPP), Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) pamoja na mdondo/kideri kwa kuku ili kukuza soko la ndani na nje ya nchi. Mwongozo pia unaainisha mikoa itakayotekeleza zoezi la utambuzi wa mifugo sambamba na uchanjaji kwa mwaka 2024/2025.

### 2.2 Malengo Mahsusi ya Mwongozo

a) Kuelezea umuhimu na faida ya kuchanja mifugo na utambuzi wa mifugo,
b) Kuelezea utaratibu wa upatikanaji wa chanjo, vifaa vya kuchanjia, hereni na utaratibu wa uchanjaji na uvalishaji hereni, na
c) Kufafanua majukumu ya kila mdau katika Kampeni ya chanjo kitaifa.

## 3.0 CHIMBUKO LA MWONGOZO

Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya Mwaka 2006; Sera ya Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binfasi ya 2009 (*National Public-Private Partnership*, 2009), Waraka wa Rais Namba 1 wa Mwaka 2002; Hotuba ya Rais ya mwezi Novemba 2020 wakati anazindua Bunge la 12 na Ilani ya CCM 2020-2025 zimetoa mwelekeo kwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kutoa huduma za mifugo ikiwemo utoaji wa chanjo. Pia, utoaji wa huduma ya chanjo kwa kutumia Sekta ya Umma na Sekta Binafsi unasimamiwa na Sheria Na. 17 ya

Magonjwa ya Wanyama (*The Animal Disease Act*) ya Mwaka 2003, na Sheria Na. 16 ya Veterinari (Veterinary Act) ya Mwaka 2003 ambazo kwa pamoja zinasimamia udhibiti wa magonjwa na watoa huduma za mifugo nchini. Aidha, Sheria ya Utambuzi Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010 inaelekeza juu ya utekelezaji wa zoezi utambuzi wa mifugo. Vile vile, Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008 na Marekebisho yake ya Mwaka 2010, inasimamia haki na ustawi wa wanyama, ikiwemo kukingwa dhidi ya magonjwa. Vilevile ina mchango wake katika mifumo ya utoaji huduma ya afya ya wanyama. Aidha, Kanuni za Chanjo na Uchanjaji za Mwaka 2020 zinazosimamia chanjo na uchanjaji zinatambua na kuainisha majukumu na mipaka ya wataalamu wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma na wadau wengine wa pembejeo, wafugaji katika utoaji na ushiriki kwenye zoezi la chanjo. Hivyo, kwa kuzingatia Sera za kitaifa, Sheria na Kanuni tajwa hapo juu; na maelekezo mbalimbali ya kitaifa, mwongozo huu unatoa utaratibu wa utoaji wa huduma ya chanjo (Uchanjaji) kwa kutumia ushirikishwaji wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Lengo ni kuwa na utaratibu mzuri unaotoa majukumu na wajibu wa kila mdau katika kutoa huduma ya chanjo za wanyama nchini.

## 4.0 UMUHIMU WA CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO

### 4.1 Umuhimu wa chanjo

Umuhimu wa chanjo dhidi ya magonjwa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP), Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) pamoja na mdondo wa kuku ni pamoja na:

a) Ni njia ya uhakika ya kulinda afya ya wanyama;
b) Kudhibiti milipuko ya magonjwa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP), Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) pamoja na mdondo wa kuku;
c) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo yaliyo bora na salama;
d) Kuongeza kuzaliana kwa mifugo na kukua haraka;
e) Kuepuka hasara inayotokana na kutibu mifugo iliyougua na vifo vinavyotokana na inayokufa;
f) Kuwa na mifugo yenye ubora ambayo itapata soko na bei nzuri ndani na nje ya nchi;
g) Kupata malighafi bora za viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo; na

h) Kupunguza uwezekano wa kuongezeka kwa usugu wa vimelea dhidi ya dawa zinazotumika katika matibabu.

### 4.2 Faida za Utambuzi wa mifugo

Faida za Utambuzi wa mifugo ni pamoja na:

a) Kukidhi matakwa ya soko la kimataifa,
b) Kuiwezesha Serikali na Wadau kuweka mipango madhubuti ya kuboresha huduma kwa mifugo,
c) Kuwezesha bima na mikopo kwa wafugaji, na
d) Kudhibiti wizi wa mifugo.

## 5.0 URATIBU WA KAMPENI YA CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO

### 5.1 Upatikanaji wa chanjo na vifaa vya kuchanjia

Chanjo na vifaa vya kuchanjia vitanunuliwa na serikali kupitia kwa wazabuni. Wazabuni watafikisha chanjo na vifaa hivyo makao makuu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa baada ya kuwasiliana na waratibu wa Kampeni ya chanjo wa mikoa na Halmashauri husika. Aidha, kila Halmashauri itapaswa kuwa jokofu/majokofu yenye sifa za kutunza chanjo husika.

Chanjo na vifaa vya kuchanjia vikishafikishwa makao makuu ya Halmashauri vitapokelewa na Mratibu wa Chanjo wa Halmashauri kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kufuata taratibu za manunuzi za Serikali. Chanjo zitahifadhiwa kwenye majokofu na kutolewa kwenda kwenye vituo vya kuchanjia siku ya chanjo kwa kuzingatia utaratibu wa kutunza na kusafirisha chanjo husika. Aidha, mratibu wa chanjo wa Halmashauri atakuwa na jukumu la kutunza kumbukumbu ya aina na idadi ya chanjo zilizotolewa na zilizotumika kila kituo na kuzitolea taarifa.

Mratibu wa chanjo wa Halmashauri atagawa vifaa vya kuchanjia kwa wataalamu wanaohusika uchanjaji uwandani kwa kuzingatia mahitaji kwa kila timu ya uchanjaji.

### 5.2 Upatikanaji wa Hereni na vifaa vya utambuzi wa Mifugo

Hereni na vifaa vya kuwekea hereni vitanunuliwa na serikali kupitia kwa wazabuni. Wazabuni watafikisha hereni na vifaa hivyo makao makuu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mikoa inayohusika baada ya kuwasiliana na waratibu wa Kampeni ya chanjo wa mikoa na Halmashauri husika (*angalia utangulizi*). Hereni na vifaa vya kuwekea hereni vitatolewa kwenda kwenye vituo husika. Aidha, mratibu wa chanjo wa Halmashauri atakuwa na jukumu la kutunza kumbukumbu ya idadi ya hereni zilizotolewa na idadi ya ng'ombe waliotambuliwa kila kituo na kuzitolea taarifa.

### 5.3 Timu za Uchanjaji

Kila Halmashauri itakuwa na idadi ya washiriki 19 wanaounda timu za uchanjaji. Aidha, kila Halmashauri itaunda timu nne (4) au tano (5) za uchanjaji zenye idadi ya washiriki wanne (4) au watano (5) kama inavyooneshwa kwenye J**edwali Na. 1.** Hata hivyo, Mratibu wa Kampeni ya Chanjo katika Halmashauri husika anaweza kubadilisha idadi hii kutegemea hali halisi ya mazingira ya ufanyaji kazi katika mazingira husika, hususan Halmashauri zile ambazo pamoja na uchanjaji, zitafanya pia zoezi la Utambuzi wa ng'ombe kwa kuvalisha hereni za kielekrtoniki.

**Jedwali Na. 1:Muudo wa timu za uchanjaji.**

| Na. | Mshiriki | Idadi | Jukumu |
|---|---|---|---|
| 1. | Wataalamu wa Mifugo wanaotambuliwa na Baraza la Veterinari | 2 au 3 | • Kuchanja mifugo kwa kuzingatia weledi,<br>• Kuangalia usalama wa chanjo (*Viability*) muda wote ikiwa ni pamoja na zinazobakia baada ya uchanjaji wa kila siku,<br>• Mmojawapo ateuliwe kuwa kiongozi wa timu,<br>• Kuvalisha ng'ombe hereni za kielektroki (*kwa Halmashauri zitakazoshiriki zoezi la Utambuzi wa ng'ombe*) |
| 2. | Mtunza takwimu na ukusanyaji maduhuli kwa | 1 | Kutoa namba za malipo (*conrol Number*) kupitia POS yenye mfumo wa TAUSI na kuhakikisha |

| Na. | Mshiriki | Idadi | Jukumu |
|---|---|---|---|
| | kutumia POS | | malipo yanafanyika |
| 3. | Utunzaji na usafi wa vifaa | 1 | Kutunza, kusafisha na kutakasa vifaa vya chanjo (*Disinfection*) |

Katika kutekeleza majukumu yake kwenye vituo vya uchanjaji, timu zitashirikiana na viongozi wa vijiji/mitaa ambapo kazi ya uchanjaji inafanyika. Viongozi hao ni Mtendaji na Mwenyekiti wa Vijiji/mitaa au vitongoji ambao majukumu yao yatakuwa ni kuhamasisha na kusimamia ujenzi/ukarabati wa vibanio pamoja na kuhakikisha mifugo yote inayohusika inafikishwa kwenye eneo la kuchanjia.

Aidha, Mratibu wa chanjo wa Halmashauri ataandaa na kuwasilisha orodha ya washiriki wa timu za wachanjaji na washiriki wengine kwa mratibu wa chanjo wa mkoa ambaye atawasilisha orodha hiyo Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia vituo vya mifugo vya Kanda (*Zonal Vterinary Centers-ZVCs*) kwa ajili ya malipo. Taarifa hiyo itawasilishwa kwa utumia **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Orodha ya Taarifa za washiriki wa Kampeni ya Chanjo ya Mifugo Kitaifa kwa ajili ya Malipo**

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Jina la Mshiriki | Jukumu* | Simu | Akaunti No | Jina la Benki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |

**NB:** ****Jukumu: Chagua kati ya haya:*** *Mkuu wa Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri, Mkurugenzi Wa Halmashauri, Mratibu wa Mkoa, Timu ya uchanjaji, Mtendaji wa kijiji au Mwenyekiti wa Kijiji*

## 5.4 Bei Elekezi ya chanjo na Uvalishaji Hereni

Kufuatia Serikali kuweka ruzuku katika kampeni ya kitaifa ya utoaji wa chanjo gharama za chanjo kwa kila mnyama itakuwa kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 3.** Aidha, zoezi la utambuzi na **uvalishaji hereni za kielektroniki litafanyika kwa ng'ombe tu na halitalipiwa**

**Jedwali Na. 3: Bei Elekezi ya chanjo**

| Na | Aina ya Chanjo | Mifugo inayochanjwa | Gharama kwa dozi moja bila ruzuku (Tzs) | Gharama baada ya ruzuku ya Serikali (Tzs) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) | Ng'ombe | 1,000 | 500 |
| 2 | Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) | Mbuzi na Kondoo | 600 | 300 |
| 3 | Mdondo wa kuku (ND | Kuku | 50 | 0 |

### 5.5 Utaratibu wa kukusanya fedha za Uchanjaji

Fedha zitakusanywa na Mtunza takwimu/Mkusanya maduhuli aliyeteuliwa Halmashauri husika kwa kutumia POS za Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye mfumo wa ukusanyaji fedha wa TAUSI. Aidha, fedha zote zitakusanywa na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uendelevu wa kampeni awamu zinazofuata.

### 5.6 Gharama za uendeshaji na malipo kwa washiriki wa Kampeni

Wizara ya Mifugo na Uvuvi itagharamia ulipaji wa posho kwa washiriki na wasimamizi wa Kampeni ambao ni pamoja na Mkuu wa Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri, Mkurugenzi Wa Halmashauri, Mratibu wa Kampeni ya chanjo Mkoa, Wachanjaji, Mtendaji/Mwenyekiti wa Kijiji/mtaa/kitongoji.

### 5.7 Usimamizi

Jukumu la Uhamasishaji, usimamizi na uangalizi wa mwenendo wa Kampeni ya Chanjo Kitaifa katika ngazi ya Halmashauri litakuwa chini ya uangalizi wa viongozi wakuu katika Halmashauri husika ambao ni Mkuu wa Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi wa Halmashauri.

## 6.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA KAMPENI YA CHANJO YA MIFUGO KITAIFA

Mambo muhimu mengine muhimu ya kuzingatia wakati wa utekelezaji wa kampeni ya chanjo ya mifugo kitaifa ni pamoja na haya yafuatayo:

a) Kuhakikisha muda wote unalinda mnyonyoro barid kwa ajili ya kutunza ubora wa chanjo husika hadi inapotumika kwa mnyama;
b) Kupima wanyama kabla na baada ya kuwapatia chanjo kubaini kiwango cha kinga kwa wanyama ili kubaini ufanisi wa chanjo husika;
c) Wataalam kuzingatia weledi na miiko ya kitaalamu wakati wa utoaji wa chanjo;
d) Kulenga kuchanja wanyama wote wanaostahili kuchanjwa dhidi ya ugonjwa husika;
e) Uwepo wa elimu kwa wafugaji na wadau wengine juu ya faida za chanjo; na
f) Uwepo wa usimamizi imara, utoaji taarifa na ufuatiliaji.

## 7.0 MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI

### 7.1 Wizara ya Mifugo na Uvuvi

a) Kuandaa mwongozo wa Kampeni ya chanjo kitaifa na utambuzi wa mifugo pamoja na kuusimamia,
b) Kutafuta fedha za kuendesha kampeni ya chanjo za mifugo kitaifa na utambuzi wa mifugo,
c) Kuratibu Kampeni ya chanjo kitaifa, utambuzina kutoa utaalamu.
d) Kununua chanjo, vifaa vya uchanjaji na hereni za kielektroniki;

### 7.2 Majukumu ya OR-TAMISEMI

a) Kuzisimamia Sekretaiet za mikoa katika kusimamia na kuratibu kampeni ya Mifugo ya Chanjo kitaifa katika Mikoa yao,
b) Kuratibu Mawasiliano kati ya Wizara ya Mifugo na uvuvi pamoja Sekretariei za mikoa na Mamlaka za Serikali za mitaa kutekeleza Kampeni ya chanjo ya Mifugo Kitaifa.

### 7.3 Majukumu ya Vituo vya kanda (ZVCs/TVLAs)

a) Kushirikiana na Halmashauri zilizo katika maeneo husika kwa kutoa msaada wa kitaalamu kuhusu chanjo na uchanjaji
b) Kukusanya sampuli kwaajili ya kufanya tathmini ya kinga mwili ya wanyama kwa magonjwa yaliyoainishwa kabla na baada ya zoezi la uchanjaji;
c) Kufanya ufuatiliaji wa matukio ya magonjwa yaliyoainishwa kabla, wakati na baada ya kampeni ya chanjo ya Mifugo kitaifa.

### 7.4 Majukumu ya Ofisi za Mikoa (RS)

a) Kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kuratibu kampeni ya Mifugo ya Chanjo katika Mkoa,
b) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Kampeni ya mifugo kitaifa na kuwasilisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi,

### 7.5 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

a) Kuhakikisha mifugo yote inapata chanjo kwenye Halmashauri husika,
b) Kuhakikisha vifaa vya mnyororo baridi katika Halmashauri husika vinapatikana,
c) Kuratibu na kutekeleza zoezi la chanjo kwa kushirikisha watoa huduma binafsi, wataalam walio nje ya ajira rasmi na wataalamu walioko katika Halmashauri katika kuleta ufanisi,
d) Kuhamasisha na kuwaelimisha wafugaji na wadau wengine kuhusu umuhimu wa kila mfugaji kuchanja mifugo;
e) Kuhakikisha uwepo wa vitendea kazi na miundombinu inayohitajika katika kampeni ya chanjo ya Mifugo kitaifa,
f) Kutunza na kutoa taarifa za chanjo na uchanjaji
g) Kuhakikisha kuwa wafugaji wote wanachanja kwa kuzingatia Sheria, ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wale wanaokaidi kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali;

### 7.6 Majukumu ya Msambazaji wa chanjo

a) Kufuata maelekezo na taratibu zote zilizowekwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mamlaka nyingine za Serikali juu ya usalama na usambazaji wa chanjo;
b) Kusambaza chanjo zilizothibitishwa ubora na kusajiliwa ama kuruhusiwa kutumika na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na Kurugenzi ya Huduma za Mifugo (DVS);
c) Kuhakikisha kuwa chanjo zote zinatunzwa katika mnyororo baridi ili kulinda ubora wake;

### 7.8 Majukumu ya Serikali ya Kijiji au Mtaa

a) Kuandaa vibanio na kuweka mazingira wezeshi ya kufanyika kwa utoaji huduma za chanjo,
b) Kushirikiana na vyama vya wafugaji, watu maarufu na viongozi wa mitaa kuhamasisha umuhimu wa chanjo kwa wafugaji wote na kuhakikisha kila mfugaji anashiriki kikamilifu kwenye zoezi la chanjo,
c) Kuhakikisha wafugaji wote wanapeleka mifugo yao kwenye vituo vya chanjo kulingana na ratiba ya chanjo;
d) Kutunza daftari la kumbukumbu za chanjo katika mifugo yao kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Mifugo,
e) Kutoa taarifa kwa Afisa Mifugo wa Kata, Kijiji, Mtaa au Wilaya pale inapotokea baadhi ya wafugaji kukaidi kuchanja mifugo yao na inapowezekana kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kutumia Kanuni za Chanjo na Uchanjaji za Mwaka 2020.

### 7.9 Majukumu ya Vyama vya Wafugaji

a) Kuwaunganisha wafugaji kupitia vyama husika ili washiriki zoezi la chanjo, na
b) Kushirikiana na Serikali katika ngazi zote kuhamasisha na kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu mwongozo huu na faida za uchajanjaji na utambuzi wa mifugo.

### 7.10 Majukumu ya mfugaji

a) Kushiriki katika kuandaa eneo na miundombinu ya kutolea huduma ya chanjo;

b) Kushirkiana na vyama vya wafugaji na viongozi wa Vijiji au Mitaa kuhamasisha umuhimu wa chanjo kwa wafugaji wengine katika zoezi la chanjo;

c) Kupeleka mifugo kwenye vituo vya chanjo kulingana na ratiba ya chanjo;

d) Kulipia gharama za chanjo kama inavyoelekezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ama uongozi wa Halmashauri kwa maeneo husika na;

## 8.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO

Mwongozo huu wa Kampeni ya chanjo ya Mifugo kitaifa kwa mwaka 2024/2025 ni Mahususi kwaajili ya uchanjaji mifugo kitaifa kwa magonjwa ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Sotoka ya Mbuzi na kondoo na Mdondo wa kuku. Mwongozo huu utaanza kutumika mwezi Februari 2025. Tunatoa wito kwa wadau wote wanaohusika na Kampeni hii kuzingatia maelekezo yaliyo katika Mwongozo huu ili kuweka usawa wa utekelezaji kitaifa na kuepuka kukiuka Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo kwa nia ya kuleta ufanisi wa Kampeni.